OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI

Simu: 0768 906072/ 0757 911531 (Mkuu wa shule)
0757 954275 (Makamu mkuu wa shule)

Shule ya Sekondari Bunazi,
S.l.p79,
KYAKA- MISSENYI.

Juni, 2018.

Kumb. Na. BSS…….
Ndg: …….
……..
……..

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUNAZI KIDATO CHA TANO MWAKA 2018.

Jumuiya ya wafanyakaziwa Shule ya Sekondari Bunazi, wanafunzi pamoja na mimi binafsi tunafurahi na kukupongeza kupata bahati kubwa ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha**TANO** katika Shule hii. Tunakukaribisha hapa shuleni kwa moyo mkunjufu. Shule ya Sekondari Bunazi iko Wilayani Missenyi, Mkoa Kagera. Unaposafiri kutoka nyumbani kwako njoo hadi stendi kuu ya mabasi ya mjini Bukoba. Kutoka Bukoba Mjini panda gari la kuelekea Mutukula ambapo utamwomba Conductorakutelemshe kibao cha Shule ya Sekondari Bunazi ambacho kiko barabarani umbali wa ¾ km kutoka makao makuu ya Wilaya. Kama una mizigo mingi unaweza kushuka kituo chaHiace cha Bunazi na kupanda pikipiki ambapo kila pikipiki si zaidi ya Tshs.500/=

Pamoja na pongezi hizo napenda kukujulisha mambo muhimu yafuatayo:-

1. Kwa kuzingatia azma ya Sera ya Elimu ya kuhamasisha wazazi kuchangia gharama za uendeshaji wa Elimu (kidato cha tano na sita) kama vifaa vya ofisini,marekebisho ya majengo ya shule, vifaa vya madasanikama madawati, mzazi anatakiwa kulipa gharama zifuatazo:-

a) MAHITAJI YA SHULE

i. **Karo:-** Unatakiwa kulipa karo ya shule Tshs. 70,000/= kwa mwaka. Waweza kulipa karo yote kwamkupuo mmoja aukulipa karo kwa awamu mbili. Muhula wa I-Tshs. 35, 000/= na muhula wa II-Tshs. 35,000/=. Karo ilipwe kupitia benki ya NMB kwa akaunti na. 3261100008 Bunazi Secondary School Recurrent A/Cna kuleta stakabadhi (Pay in Slip) ya malipo hayo kwa Mhasibu ili akupe stakabadhi ya serikali (Hundi binafsi hazitapokelewa).

ii. **Taaluma**- Tshs. 20,000/= kwa mwaka, unaweza kulipa kwa awamu mbili.

iii. **Fedha za taadhali** (Caution Money) – Tshs 5,000/= Mara moja kwa miaka miwili (Haitarejeshwa).

iv. **Fedha za Matibabu** – Tshs 30,000 Hii ni kwa ajili ya bima (CHF) na matibabu ya huduma ya kwanza itolewayo hapa shuleni. Ilipwe mara moja tu kwa miaka miwili.

v. **Kitambulisho**- Tshs 5,000/=

vi. **Nembo ya Shule** – Tshs. 2,000/=

vii. **Mchango wa mahitaji ya ofisini:** Unatakiwa kuleta Bunda moja ya karatasi za Computer “A4” (Ream) kwa ajiliya kuchapa mitihani na mazoezi vinavyofanyika shuleni. Iletwe Ream moja kila mwaka.

viii. **Ulinzi –** Tshs. 5,000/= Ilipwe kila mwaka.
ix. **Mchango wa dawati –** Tshs . 30,000/= Ilipwe mara moja tu.
x. **Mchango wa mpishi** - Tshs. 20,000/= Ilipwe kila mwaka.
xi. **Mchango wa ukarabati** - Tshs 20,000/= Ilipwe mara moja kwa miaka miwili.
xii. **Fedha za UMISSETA** – Tshs. 1,500/= kila mwaka au 3,000/= mara moja.
xiii. **Mlezi (Matron)** – Tshs. 10,000/= Ilipwe kila mwaka.
xiv. **Vifaa vya usafi na Mazingira ya shule na Elimu ya kujitegemea: Unatakiwa kuleta vifaa vifuatvyo**:-

1) Jembe moja na mpini wake
2) Fyekeo moja jipya lililonolewa
3) Rato (Rake) moja yenye mpini
4) Ndoo yenye ujazo wa lita 20
5) Soft bloom/ Hard bloom/ Squeezer.

xiv. **Picha tatu:** (Passport size) za rangi. Unatakiwa kuleta picha tatu (passport size) na kuzikabidhiwakati wa kuripoti shuleni.

xv. **SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE:-**

1) Sketi itapatikana hapa shuleni kwa thamani ya Tshs. 16,000/= @ sketi. Sketi mbili ni Tshs. 32,000/=. Hii ni kuepuka utofauti wa mishono na rangi ya kitambaa pamoja na ugumu wa kitambaa.
2) Njoo na mashati mawili meupe ya mikono mirefu (Tetron) – yasiwe ya mitumba.
3) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ununuzi wa sweta ya sare ya shule kwa ajili ya kujikinga na baridi.
4) Shilingi 3,000/= kwa ajili ya ununuzi wa tai ya sare ya shule.
5) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ununuzi wa T-Shirt. Pia uje na sketi mbili za kijani (Kitambaa cha sukari, malinda 16). Sare hii ni ya kuvaa baada ya muda wa darasani.
6) Uje na jozi mbili za Viatu vyeusi vya ngozi (visivyochongoka, visiwe na sori ndefu/ kubwa sana) na soksi Nyeupe ndefu jozi mbili au zaidi. Viatu viwe vinafungwa kwa kamba.
7) Uje na nguo za michezo (Track Suits) za rangi ya blue bahari na T-Shirt rangi nyekundu pamoja na raba) Zitavaliwa wakati wa michezo uwanjani tu.
8) Uje na Toilet Paper dazeni moja.
9) Shati ya mikono mirefu summer blue (Bluu Bahari) Shati hii itavaliwa tu wakati wa ziara za nje ya mazingira ya shule.
10) Wasichana wa dhehebu la Kiislamu wanaruhusiwa kuvaa Hijabu inayofanana na rangi ya shati (Nyeupe) iliyoshonwa vizuri.

1. TANBIHI.

- Hutakiwi kuja na Shati au Suruari au nguo yoyote tofauti na hizo ulizoagizwa.
- Kumbuka kwamba HUTAPOKELEWA endapo utashindwa kutimiza mahitaji yote yaliyoorodheshwa hapo juu. Ili kuepukana na usumbufu wa kurudishwa nyumbani kutokana na kutotimiza mahitaji, unashauriwa kukamilisha mahitaji haya kabla ya kuripoti shuleni. Fedha zote ziwekwe katika Akaunti Na. 3261100008 Bunazi Secondary School (**NMB BANK**).
- Pamojana mahitaji mengine uje na nguo za ndani dozen 1 na mahitaji mengineyo ya kike.

- **USAFIRI:** Itakubidi ujigharimie kwa usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Au sababu yoyote nje ya likizo.
- **CHETI KUTOKA KWA DAKTARI:**Itakubidi urudishe fomu iliyoambatanishwa ikiwa imethibitishwa na Daktari wa Hospital ya Serikali ya Halmashauri ya Wilaya au Mkoa kuwa umepimwa na kwamba unaweza kumudu masomo nakazi za nje bila matatizo.

- **URAIA:** Unatakiwa kuleta shuleni nakala ya CHETI CHA KUZALIWA (Birth Certificate).
- **KUKUBALI MASHARITI YA SHULE:** Ninaambatanisha sheria za Shule na fomu ya kukubali kutii kwa dhati Sheria hizo pamoja na fomu nyingine ya maelezo yako binafsi. Zisomwe kwa makini Sheria hizo, ukizikubali uweke saini yako fomu ya kukubali kujiunga mbele ya mzazi au mlezi wako na uziwasilishe fomu hizo Shuleni.

2. VIFAA BINAFSI: Unatakiwa uje navifaa vifuatavyo vya kukusaidia uwapo shuleni.

i. GODORO moja la Sponge size Futi 2½kwa sita (2½ X 6) (Godoro imara).
ii. Shuka MBILI - RANGI YA PINK na Blanket moja kwa ajili ya baridi usiku.
iii. MTO (1) na FORONYA mbili za rangi ya PINK na Chandarua.
iv. JACKET jeusi (sio koti) kwa ajili ya kujikinga na mvua. Pia kujikinga na baridi kwa mgonjwa wa kifua na mwenye Cheti cha Daktari ambalo lazima livaliwe juu ya Sweta ya shule.
v. KANDA MBILI, TAULO, NDOO ya maji yako binafsi kwa ajili ya kuogea au kufulia tu.
vi. VIFAA VYA DARASANI: Kalamu za wino na Risasi, Kifutio na rula, Daftari (Counter book) 10 na mkebe bila kusahau Kamusi ya Kiingereza (Advanced learners dictionary).
vii. VITABU Muhimu vya masomo unayochukua.
viii. Kijiko, Sahani na Kikombe na bakuli (visiwe vya plastiki).

3. KUFIKA SHULENI:

Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe itakayotangazwa. Mara ufikapo shuleni, ripoti mara moja ofisini kwa Mkuu wa Shule ukiwa na mahitaji yote ya shule uliyojulishwa hapo juu tayari kwa kukaguliwa. Ukichelewa kuripoti zaidi ya wiki mbili (2) bila sababu maalumu baada ya shule kufunguliwa, unaweza kupoteza nafasi yako. Siku za kuripoti wanafunzi ni**Jumatatu mpaka Ijumaa kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 12.30 Jioni**.

Nakutakia kila la kheri na mafanikio tele uwapo hapa shuleni.

KARIBU SANA.

MUHIMU:

1. Michango yote ya shule ilipwe katika akaunti namba3261100008 (NMB BANK).Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye PAY IN SLIP na kuiwasilisha shuleni. Hakuna mchango ambao si muhimu.
2. Uje na kivuli cha CHETI CHA KUMALIZA KIDATO CHA NNE (School Leaving Certificate) pamoja na RESULT SLIP yako ya kidato cha nne.

Nakutakia maandalizi mema.

MKUU WA SHULE.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI
SHULE YA SEKONDARI BUNAZI
SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1977. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia Kanuni na Sheria hizi kwa kipindi chote utakachokuwa hapa.**(Maelekezo mengine utapewa mara ufikapo shuleni).**

i. Kila Mwanafunzi ni lazima kuvaa nguo rasmi za shule (School uniform) wakati wote uwapo shuleni na mahali pengine atakapotakiwa kufanya hivyo.
ii. Ni muhimu na wajibu kwa kila mwanafunzi kuwahi bila kuchelewa mahali popote atakapohitajika darasani, kazini, mstalini n.k.
iii. Juhudi katika kazi za mikono, madarasani na katika michezo ni wajibu wa kila mwanafunzi. Uzembe katika shughuli hizi hauruhusiwi kabisa.
iv. Kila mwanafunzi wa shule hii ni budi aombe ruhusa, endapo atakosa kuwapo shuleni.
v. Kila mwanafunzi ni wajibu kujiheshimu yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine kama anavyopenda kuheshimiwa.
vi. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza na kulinda siha na usafi wake binafsi na wa mazingira yote ya shule nje na ndani ya madarasa, vyoo n.k.
vii. Vitendo vyovyote vya kushiriki au kushawishi migomo ya aina yoyote shuleni ni marufuku kabisa.
viii. Ugomvi au kupigana, kuleta fujo darasani, lugha za matusi, kashfa kwa wenzako au wananchi ni mwiko kabisa.
ix. Vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba ni lazima uvihudhurie bila kukosa pamoja na shughuli za nje ya darasa.
x. Kila mwanafunzi ni sharti aepuke na kuchukia vitendo vyovyote vya uongo, uzushi, wizi uasherati, ulevi, uvutaji sigara na uchoyo.
xi. Upole na utii kwa viongozi ni wajibu kwa kila mwanafunzi, ubishi wenye lengo la kukwepa na kutimiza wajibu ni marufuku kabisa!
xii. Makoti, vibandiko, vizibau, kofia kanda mbili, viatu vya wazi, mikanda mipana, bukta haviruhusiwi kamwe kuvaliwa bwaloni, darasanina wakati mwanafunzi awapo ndani ya vazi la shule.
xiii. Lugha inayotumika hapa shuleni ni Kiingereza tu.
xiv. Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (Preparation) ni lazima.
xv. Ni marufuku kuwa na simu ya mkononi (Mobile Phone), Kompyuta (Laptop) na I Pad USIJE NAVYO SHULENI.
xvi. Ni marufuku kupeleka chakula mabwenini.
xvii. Ni marufuku kumiliki kifaa chochote kinachoweza kusaidia mwanafunzi kufanya biashara yoyote awapo shuleni. MfanoCamera, Kuuza vyakula au vinywaji.
xviii. Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele.
xix. Makosa yafuatayo yanaweza kukufanya ufukuzwe ama kutolewa shuleni.
   a. Wizi.
   b. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kubeli n.k.
   c. Ubakaji.
   d. Kudharau Bendera ya Taifa.
   e. Kuoa au kuolewa.
   f. Uharibifu wa makusudi wa mali ya Umma.
   g. Kugoma, kuchochea na kuongoza/ kuvuruga Amani na usalama wa shule.
   h. Kukataa adhabu.

i. Kupigana au kupiga.
j. Utoro.
k. Kushawishi/ kushiriki katika migomo.
l. Kutofanya mitihani na mazoezi.
m. Mapenzi ya ngono na wanafunzi wenzako au watu wengine ndani nan je ya shule (Uasherati na Ushoga).
n. Kumpa mwanafunzi wa kike mimba au kubeba mimba.
o. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

AHADI YAKO:

Nimezisoma sheria/ kanuni hizi na kuzielewa, nitazitimiza/ sitazitimiza.

JINA LA MWANAFUNZI SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

…… ……. ……

Mimi …… (Mzazi/ Mlezi) nathibitisha kuwa niko tayari kumlipia mwanafunzi …… kidato cha …… karo na michango ya shule yote itakayoidhinishwa na Bodi ya shule au Kamishena wa Elimu kwa ajili ya maendeleo ya shule na mwanafunzi. Aidha naahidi kuwa ifikapo kila mwaka wa shule (Juni na Desemba) nitakuwa nimemaliza deni la mwaka huo.Karo na michango mingine nitalipa mimi …… wa S.L.P. …….. Sahihi ya Mzazi/ Mlezi ……..... Namba ya simu …… Tarehe ……
Tafadhali soma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII.

…….
GODELIVA K. NGIRWA
MKUU WA SHULE.

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili: ……..
2. Anwani ya nyumbani: ……
3. Tarehe ya kuzaliwa: …… Mahali ulipozaliwa: Wilaya ……. Tarafa ……. Kata …… Kijiji/ Mtaa ……
4. Shule ya Sekondari ulipotoka: …….. anwani …….
5. Dini yako: …….
6. Jamaa katika familia yako
   a. Jina la Baba: …….. Namba yake ya simu …… Anaishi/ Haishi
      Kazi yake: ……..
   b. Jina la Mama: …… Namba yake ya simu …… Anaishi/ Haishi.
      Kazi yake: ……..
   c. Jina la Mlezi: …….. Namba yake ya simu ……... Anaishi/ Haishi.
      Kazi yake: ……..
      Uhusiano wake na wewe: ……..

7. Mimi …….. (Mwanafunzi) nadhibitisha kuwa taarifa nilizozitaja hapo juu ni za kweli.
   Sahihi ya Mwanafunzi: ……
8. Mimi ……. (Mzazi/ Mlezi) wa mwanafunzi nimehakikisha kuwa taarifa zilizotajwa hapo juu ni za kweli.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi …….
IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI.

Anwani ya Mzazi/ Mlezi …….
Namba ya simu ……. Tarehe ……

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Bunazi,
S.L.P 79,
KYAKA.

Ndg,

YAH: MALEZI YA MTOTO WANGU …….. KIDATO CHA …… MWAKA ……

Nimezisoma sheria na kanuni za shule na kuzielewa vizuri. Napenda kuhakikisha kwamba mimi mzazi/ mlezi wa mtoto huyu niko tayari/ siko tayari kusaidiana na shule katika jitihada zake za kumjengea mtoto wangu nidhamu ya dhati. Katika hali hiyo nitajitahidi/ sitajitahidi kumwogoza ili:-

i. Awahi shuleni na awe kwenye shughuli zake kulingana na taratibu za shule.
ii. Asikose kuhudhuria shuleni kama hakuna sababu kubwa ya kumzuia.
iii. Asijihusishe na matendo ya utoro, uzururaji, matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vinginevyo vinavyoweza kumzuia kuendelea na shule.
iv. Asipuuze au kukataa kuhudhuria miradi ya shule kama vile kilimo cha nyanya, kuhudumia mifugo na kutunza usafi wa mazingira.
v. Akazanie masomo kwa lengo la kufaulu mitihani.

…… ……
Jina kamili la Mzazi/ Mlezi Sahihi

AHADI YA MZAZI/ MLEZI YA KUWA NA MAHUSIANO BORA NA SHULE.

Shule ya Sekondari Bunazi,
S.l.p 79,
KYAKA.
TAREHE …….

MAHUSIANO NA MALEZI (MM)

1. Wazazi/ Walezi kuwa barua yenye kuleta ujumbe muhimu wanafunzi kama kumwombea ruhusa aje nyumbani kwa shughuli muhimu/ maalumu ni lazima iandikwe na mzazi/ mlezi aliyeandikishwa shuleni.

2. Kuhusu masuala mbalimbali yanyohusu mwanafunzi, shule haitakuwa tayari kuyajadili na mtu/ ndugu yeyote atakayejitokeza. Masuala yoyote kuhusu mwanafunzi yatajadiliwa au mawasiliano yatafanyika kati ya shule na mzazi/ mlezi aliyeandikishwa shuleni wengine hawatakubaliwa. Labda kwa idhini maalumu itakayoandikwa na mzazi/ mlezi mwenyewe.

i. Jina la Baba ……...
Kazi ……...
Anwani…….....

ii. Jina la Mama …….
Kazi ……...
Anwani ……..

iii. Jina la Mlezi ……..
Mlezi ni Yule mtu uliyemteua kama haupo kukuwakilisha katika maswala ya mwanafunzi huyu shuleni.
Kazi ……...
Anwani ……..

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi:……
Tarehe …….
NB: (Jaza sehemu zote tatu kwa watu watatu tofauti).

VITABU

HISTORY REFERENCE BOOKS

1. CK. Shibitali (2015, 2016, 2017 edition) Contemporary world Events.
2. D.E. Butendeli (2016) Major trands in world history from Medieval era to Present advanced level Comprehensive Note. History paper two.
3. Oxford Advanced Learners history form 5.

GEOGRAPHY

1. Advanced Geography paper 1.
2. Advanced Geography paper 2.
3. Advanced Physical Geography.
4. Advanced Human Geography.
5. Land forms in Africa.
6. Advanced Practical Geography.

KISWAHILI

1. Nadharia ya lugha Kiswahili moja kidato cha tano na sita – Nyambali Nyangwine
2. Nadharia ya lugha Kiswahili mbili kidato cha tano na sita fasihi kwa ujumla
3. Tahakiki ya vitabu teule kidato cha tano na sita.

GENERAL STUDIES

1. Comprehensive book for advanced level secondary schools – Mwajabu B. Mruma
2. General Studies – Nyambali Nyangwine
3. General Studies Alive – Zisti Kamili